**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU RATIBA YA KUTOA FOMU UTEUZI WA WAGOMBEA WA KITI CHA RAIS NA MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

*Ndugu wananchi!*

Mnamo tarehe 26 Julai, 2025, kwa kuzingatia masharti ya ibara ya 41(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ikisomwa pamoja na kifungu cha 41(1) na 49(1) vya Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi ilitangaza Ratiba ya Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2025.

Ratiba hiyo ilionesha tarehe za utoaji wa fomu za wagombea wa Kiti cha Rais na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wagombea wa nafasi ya Ubunge na Madiwani.

*Ndugu wananchi!*

Kwa mujibu wa ratiba ya uchaguzi iliyotangazwa na kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 34(1) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, kikisomwa pamoja na kanuni ya 20(1) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025 Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi kuanzia kesho tarehe **09 Agosti, 2025** hadi tarehe **27 Agosti, 2025** itaanza kutoa fomu za uteuzi kwa wagombea wa Kiti cha Rais na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Zoezi hilo la utoaji wa fomu litafanyika kwenye ofisi za Tume Jijini Dodoma.

*Ndugu wananchi!*

Hadi leo tarehe 08 Agosti, 2025, tumepokea barua kutoka katika vyama vya siasa kumi na nne (14) vikiainisha tarehe na muda ambao wanachama wa vyama vyao waliowapendekeza kugombea nafasi za Kiti cha Rais na Makamu wa Rais watafika ofisi za Tume zilizopo eneo la Njedengwa Jijini Dodoma kwa ajili ya kuchukua Fomu za Uteuzi.

Vyama hivyo ni:

1. Chama cha Mapinduzi (CCM)
2. National Reconstruction Alliance (NRA)
3. Alliance for African Farmers Party(AAFP)
4. Chama cha MAKINI
5. The National League for Democracy (NLD)
6. United Peoples' Democratic Party (UPDP)
7. African Democratic Alliance Party (ADA - TADEA)
8. Union for Multiparty Democracy (UMD)
9. Tanzania Labour Party (TLP)
10. Chama Cha Kijamii (CCK)
11. Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA)
12. Alliance for Democratic Change (ADC)
13. Democratic Party (DP); na
14. National Convention for Construction and Reform (NCCR - MAGEUZI)

*Ndugu wananchi!*

Hivyo, kutokana na orodha hiyo ya vyama kumi na nne (14) vilivyowasilisha taarifa za wanachama wao waliopendekezwa kuwa Wagombea wa Kiti cha Rais na Makamu wa Rais, ifuatayo ni ratiba ya utoaji wa fomu za uteuzi:

| Na. | Tarehe | Jina la chama | Muda |
|---|---|---|---|
| 1. | 09 Agosti, 2025 | Chama cha Mapinduzi (CCM) | 5:00 Asubuhi |
| 2. | 09 Agosti, 2025 | National Reconstruction Alliance (NRA) | 8:00 Adhuhuri |
| 3. | 09 Agosti, 2025 | Alliance for African Farmers Party (AAFP) | 10:00 Alasiri |
| | | | |
| 4. | 10 Agosti, 2025 | Chama cha MAKINI | 3:00 Asubuhi |
| 5. | 10 Agosti, 2025 | The National League for Democracy (NLD) | 6:00 Adhuhuri |
| 6. | 10 Agosti, 2025 | United Peoples' Democratic Party (UPDP) | 9:00 Alasiri |
| | | | |
| 7. | 11 Agosti, 2025 | African Democratic Alliance Party (ADA - TADEA) | 3:00 Asubuhi |
| 8. | 11 Agosti, 2025 | Union for Multiparty Democracy (UMD) | 6:00 Adhuhuri |
| 9. | 11 Agosti, 2025 | Tanzania Labour Party (TLP) | 9:00 Alasiri |
| | | | |
| 10. | 12 Agosti, 2025 | Chama Cha Kijamii (CCK) | 3:00 Asubuhi |
| 11. | 12 Agosti, 2025 | Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA) | 6:00 Adhuhuri |
| 12. | 12 Agosti, 2025 | Alliance for Democratic Change (ADC) | 9:00 Alasiri |

| Na. | Tarehe | Jina la chama | Muda |
|---|---|---|---|
| | | | |
| 13. | 13 Agosti, 2025 | Democratic Party (DP) | 3:00 asubuhi |
| | | | |
| 14. | 15 Agosti, 2025 | National Convention for Construction and Reform (NCCR – MAGEUZI) | 6:30 Adhuhuri |

*Ndugu wananchi!*

Tume imeviandikia barua vyama vya siasa husika kuvijulisha kuhusu ratiba hiyo ya utoaji fomu za uteuzi.

**Aidha, ni muhimu tukumbuke kuwa, ratiba hii inahusu vyama kumi na nne (14) pekee vilivyowasilisha taarifa hadi kufikia leo tarehe 08 Agosti, 2025, hivyo iwapo vyama vingine vitajitokeza, tutaandaa ratiba husika na kuwajulisha.**

*Ndugu wananchi!*

Tunavipongeza vyama vyote vya siasa kwa kuendelea kufanya maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025. Tume kwa upande wake itazingatia katiba, sheria na kanuni wakati wote wa mchakato wa uchaguzi.

Ahsanteni sana kwa kunisikiliza.

**"KURA YAKO HAKI YAKO JITOKEZE KUPIGA KURA"**

Imetolewa leo tarehe 08 Agosti 2025; na

Kailima, R.K

**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**